**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

MKUU WA TAKUKURU MKOA
Mtaa wa Uzunguni,
S.L.P 37,
**37101 SHINYANGA,**
**Tanzania.**
Simu: (028) 2762630
Nukushi: (028) 2763358

APRILI, 2022.

# TAKUKURU SHINYANGA YABAINI DOSARI KWENYE MIRADI MINNE YA MAENDELEO INAYOTEKELEZWA MKOANI HUMO

Hii ni taarifa ya kazi zilizotekelezwa na TAKUKURU mkoa wa Shinyanga katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/2022 (Januari-Machi, 2022).

## 1. KAZI ZA KUZUIA RUSHWA.

**Ndugu Waandishi wa Habari.**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha katika miradi maendeleo kumi na nane (**18**) Mkoani Shinyanga, yenye thamani ya **Sh. 13,794,801,486** iliyoletewa fedha na Serikali. Mchanganuo wa miradi hiyo kisekta ni kama ifuatavyo: Miradi sita (6) sekta ya afya, mitano (5) sekta ya miundombinu, miwili (2) sekta ya elimu na mitano (5) sekta ya maji. Kati ya miradi hiyo 18 iliyoifuatiliwa, ilibainika kwamba miradi minne (4) ilikuwa na dosari na miradi 14 haikuwa na dosari.

Kati ya miradi minne (4) iliyokuwa na dosari miradi mitatu (3) dosari zake zilikuwa ndogo ndogo kiasi kwamba TAKUKURU mkoa wa Shinyanga ilitoa ushauri wa namna ya kuzifanyia marekebisho dosari husika kwa mamlaka husika. Miradi iliyobainika kuwa na dosari ndogo ndogo ni hii ifuatayo:

- Mradi wa ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya wasichana Butengwa,
- Ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Usule na
- Ujenzi wa barabara za changarawe zilizo chini ya TARURA katika Manispaa ya Shinyanga. Baadhi ya dosari ndogo ndogo zilizobainika kwenye miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

i) Kwenye mradi wa Barabara baadhi ya maeneo katika barabara ya Bugweto -Ipeja kutokuchongwa na kushindiliwa vizuri.
ii) Baadhi ya maeneo ya pembeni katika barabara ya Butengwa – Nin'gwa kuharibika mapema kutokana na kutokushindiliwa vizuri na kutengenezwa wakati wa mvua.
iii) Kwenye mradi wa shule mpya ya sekondari ya wasichana Butengwa tulibaini msingi ulichimbwa kwenda chini urefu wa sentimeta 70 badala ya sentimeta 90 kama BOQ inavyoonyesha.
iv) Kwenye mradi wa shule mpya ya sekondari ya Usule tulibaini kutokuwekwa njia za kupita walemavu kwenye baadhi ya majengo.

Miradi hii mitatu yenye dosari ndogondogo ilitolewa ushauri wa namna ya kurekebisha dosari zilizobainika kama ifuatavyo:

I) Kwenye mradi wa barabara za changarawe zilizo chini ya TARURA - Manispaa ya Shinyanga tumemshauri meneja wa TARURA amtake mkandarasi arudie kuchonga na kushindilia sehemu zote za barabara ya Bugweto - Ipeja na Butengwa – Nin'gwa ambazo hazijachongwa vizuri.
II) Katika mradi shule ya sekondari ya wasichana Butengwa tulielekeza msingi wa jengo uchimbwe kwa mujibu wa BOQ.
III) Katika mradi shule mpya ya sekondari ya Usule tulielekeza njia za kupita walemavu zijengwe.

Aidha, ilitolewa elimu juu ya utekelezaji bora wa miradi hasa inayotumia force akaunti kwenye maeneo ya uandikaji wa kumbukumbu za manunuzi, utunzaji wa nyaraka za miradi na utunzaji vifaa vya ujenzi.

Sambamba na kutoa ushauri huo TAKUKURU Shinyanga ilifuatilia kuona iwapo ushauri uliotolewa ulitekelezwa katika sekondari ya wasichana Butengwa. Imebainika kuwa ushauri uliotolewa umetekelezwa.

Mradi mmoja (01) kati ya hiyo 4, ambao ni mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Salawe, ulibainka kuwa na dosari hususan katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambapo uchunguzi umeanzishwa.

Miradi 18 yenye jumla ya thamani ya Sh. **13,794,801,486** iliyokaguliwa bado utekelezaji wake unaendelea na iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na mradi mmoja umeanzishiwa uchuguzi kama ilivyo elezwa hapo awali.

Sambamba na hilo kwa kipindi husika ofisi imefanya kazi tatu (3) za uchambuzi wa mfumo katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ambapo ofisi ilifanya uchambuzi kuhusu Utendaji kazi wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (**GPSA**), Tathmini ya wakala wa huduma za umeme na ufundi (**TAMESA**) katika huduma za matengenezo ya magari na uchambuzi wa mfumo juu ya mianya ya rushwa katika Usimamizi wa uchimbaji wa madini ya ujenzi na mapato yanayotokana na ntozo ya madini ya ujenzi katika ngazi ya serikali ya mitaa na Manispaa ya Shinyanga.

Katika kuboresha mifumo hiyo, ofisi ya TAKUKURU katika kipindi **cha Aprili hadi Juni, 2022** itafanya vikao vya warsha na kujadiliana na wadau namna bora ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainika katika taasisi hizo hivyo utekelezaji wa maazimio ya vikao vya warsha yanaendelea.

## 2. KAZI ZA CHUNGUZI.

**Kwa upande wa Dawati la Uchunguzi,** tumepokea taarifa 48 za malalamiko, ambapo **taarifa zinazohusu rushwa zilikuwa 35** na **zisizohusu rushwa zilikuwa 13.**

Kati ya taarifa 35 zilizohusu rushwa, taarifa 17 uchunguzi wake unaendelea, taarifa 13 uchunguzi wake umekamilika na taarifa 5 uchunguzi wake umefungwa kwa kukosa ushahidi. Taarifa 13 ambazo hazikuhusu rushwa, taarifa 4 zilihamishiwa idara nyingine na taarifa 9 watoa taarifa wake walishauriwa.

Kesi zinazoendelea mahakamani ni 18 kati ya hizo kesi mpya ni 03 na katika kipindi hicho cha Januari – Machi, kesi 06 ziliamuliwa mahakamani na kesi 4 zilishinda kwa watuhumiwa kutiwa hatiani na kulipa faini.

## 3. KAZI ZA ELIMU KWA UMMA.

Taasisi imeendelea na jukumu lake la kuelimisha umma huku ikitoa kipaumbele kuelimisha wananchi wote kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kufanya kazi zifuatazo;

| NA | KAZI ZILIZOFANYIKA | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | Semina. | 09 |
| 2. | Mikutano ya hadhara. | 04 |
| 3. | Uimarishaji wa klabu za wapinga Rushwa. | 39 |
| 4. | Vipindi vya Redio | 06 |
| 5. | Mikutano na vyombo vya habari. | 01 |
| 6. | Maonesho. | 4 |
| **Jumla ya wananchi 22,109 walielimishwa.** | | |

**TAKUSKA**

Ofisi ya TAKUKURU Shinyanga katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka 2022 kwa kushirikiana na skauti mkoa wa Shinyanga imetoa elimu kwa viongozi wa skauti wapatao 30 wa wilaya ya Kishapu ili waweze kushiriki katika usimamizi wa miradi katika maeneo yao. Aidha, kuwawezesha kuzijua mbinu za viashiria vya rushwa kwenye miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao na kutoa taarifa TAKUKURU ili iweze kuchukua hatua stahiki za kuzibiti vitendo vya rushwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA NCHINI.**

TAKUKURU (M) Shinyanga mwezi januari kuanzia tarehe 23/01/2022 hadi 29/01/2022 ilishiriki katika maonesho ya maadhimisho ya wiki ya sheria yaliyofanyika katika wilaya zote za mkoa wa Shinyanga ambazo ni Shinyanga, Kahama na Kishapu. Wananchi mbalimbali waliohudhuria banda la TAKUKURU walielimishwa na kupata wasaa wa kufahamu shughuli zinazotekelezwa na TAKUKURU na kupatiwa elimu kuhusu makosa ya rushwa. Pia, wananchi takribani 220 waligawiwa vipeperushi vyenye jumbe za rushwa, makosa ya rushwa na umuhimu wa kusimamia miradi ya maendeleo.

**MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI**

TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga kupitia wilaya ya Kahama mnamo tarehe 08/03/2022 ilishiriki katika maonesho ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Kituo cha Uwekezaji

ambayo kimkoa yaliadhimishwa wilayani Kahama. Wananchi mbalimbali waliofika kwenye banda la TAKUKURU walipatiwa elimu ya rushwa ya ngono na takribani wananchi 132 waligawiwa vipeperushi vyenye jumbe za "Ifahamu rushwa ya ngono".

**MIKAKATI YA UTENDAJI KAZI WA TAKUKURU MKOA WA SHINYANGA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI HADI JUNI 2022.**

Kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2022 ambacho ni robo ya mwisho ya mwaka wa fedha 2021/22, TAKUKURU mkoa wa Shinyanga imepanga kukamilisha majukumu yake kwa kujielekeza aidi kwenye ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kufanya chunguzi.

Mwisho napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wanahabari wote wa mkoa wa Shinyanga kwa kushiriki kwenu katika mapambano dhidi ya rushwa.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

**Imetolewa na:**

**H.M Mussa**

**Mkuu wa TAKUKURU (M) Shinyanga.**

**0738-150 196**

**0738- 150 197.**